
GOVERNMENT OF WESTERN AUSTRALIA

Department of **Local Government, Sport and Cultural Industries**
Office of **Multicultural Interests**

# Kadi ya "Nahitaji Mkalimani" ya Australia ya Magharibi
## Taarifa kwa jamii




**Kama unaona ni vigumu kuwasiliana kwa Kiingereza, kadi hii itayafanya mashirika ya Kiserikali yajue kuwa unahitaji mkalimani**

**Jinsi gani ya kutumia kadi hii?**
Andika jina la lugha unayoizungumza au kutumia mbele ya kadi kwa Kiingereza. Kama unaongea au kutumia lugha zaidi ya moja, andika hizo lugha zingine kwenye kadi ukianzia na ile unayoijua sana na kufuatisha ile usiyoijua sana. Uliza mtu aliyekupa kadi akusaidie juu ya hili kama inatakiwa.

Kama unahitaji msaada kutoka kwa mkalimani wakati unapotumia huduma ya Serikali, onyesha kadi yako kwa mfanyakazi. Watajaribu kukupangia mkalimani (uso kwa uso au kwa simu) anayeongea lugha yako.

Kama mkalimani anayeongea lugha yako ya kwanza hayupo, mfanyakazi atajaribu kutafuta mkalimani anayeongea lugha yako ya pili au ya tatu.

**Nani anaweza kupata Kadi ya Mkalimani?**
Mtu yeyote anayehitaji msaada wa kuwasiliana katika Kiingereza wakati akitumia huduma za serikali anaweza kupata kadi.

**Kadi inagharimu kiasi gani?**
Kadi ni ya bure. Ukipoteza kadi yako, unaweza kupata nyingine kwa bure.

**Naweza kupata kadi wapi?**
Kadi zinapatikana kutoka kituo cha habari za wahamiaji, watoaji huduma za jamii ya utamaduni mbalimbali, baadhi ya hospitali za serikali, shule zenye vituo vikubwa vya Kiingereza, baadhi ya halimashauri za miji, Jumuia ya Visiwi ya Australia ya Magharibi, Huduma ya Ukalimani ya Kimberley na Vituo vya Lugha ya Watu wa Asili.

Information for Communities: Swahili

**Naweza kutumia kadi kwa muda gani?**
Unaweza kutumia kadi yako kwa muda mrefu unapoendelea kuhitaji msaada wa mkalimani ili kupata huduma za Serikali. Kadi haiishi tarehe ya kutumika.

**Watu wengine wanaweza kutumia kadi yangu?**
Mtu yeyote anayeongea au kutumia lugha yako anaweza kutumia kadi yako, pamoja na ndugu yako wa familia.

**Naweza kuomba mkalimani kama sina kadi?**
Ndiyo. Bado unaweza kuomba mkalimani kwenye mashirika ya Serikali hata kama huna kadi.

**Je, nitalazimika kulipia gharama ya mkalimani?**
Hapana. Kama unaruhusiwa kutumia huduma za Serikali, shirika husika litalipia gharama za mkalimani.

**Naweza kuomba mkalimani wa kiume au wa kike?**
Unaweza kuomba mkalimani wa kiume au wa kike, lakini, hii itategemeana na sera ya shirika, hali halisi na upatikanaji wa mkalimani.

**Naweza kuomba ndugu wa familia au rafiki kuwa mkalimani?**
Hii haipendekezwi, isipokuwa kutoa taarifa za kawaida au katika hali za pekee. Kila shirika la Serikali litapima ni lini mkalimani mwenye sifa lazima, pengine au labda atumiwe kutegemeana na lengo la mawasiliano.

Rafiki au ndugu wa familia anaweza kuhusika kihisia, na anaweza kuwa hana ujuzi unaotakiwa au msimamo maalumu.

Mtu yeyote chini ya miaka 18 hatakiwi kuombwa kutafsiri.

**Je natakiwa kutaarifu shirika la huduma kabla ya muda kuwa nitahitahi mkalimani?**
Ndiyo. Isipokuwa kama ni dharura, ni vizuri kuwaarifu wafanyakazi kabla ya muda kuwa unahitaji mkalimani ili waandae utaratibu unaotakiwa.

**Je itakuwaje kama sitawaarifu wafanyakazi kabla ya muda kuwa nitahitaji mkalimani?**
Wafanyakazi watafanya wawezavyo kukusaidia.Kwa mfano, wanaweza:
- kutumia mkalimani kupitia simu, kama mkalimani wa uso kwa uso hayupo
- kukupangia muda mwingine wa kuja wakati mkalimani atakapokuwepo.
- kukupa habari au ujumbe katika lugha yako, kama ipo.
- kutumia mfanyakazi anayezungumza lugha yako, kama yupo, kupata ujumbe wa kawaida, ili kusaidia kupanga mkutano mwingine na mkalimani

**Naweza kufanya nini kama ombi langu la mkalimani limekataliwa?**
Katika baadhi ya hali shirika linaweza lisitoe mkalimani lakini linaweza kujaribu kukusaidia kupitia njia zingine (kwa mfano, kwa kukupa habari katika lugha unayoweza kuisoma. Hata hivyo, tafadhali taarifu shirika kama huwezi kusoma katika lugha yako).

Kama unahitaji mkalimani na umemwomba mkalimani lakini shirika limekataa, unaweza kutoa lalamiko kwa shirika hilo.

Kama haujaridhika na majibu ya shirika hilo, unaweza kuwasiliana na shirika la Australia ya Magharibi la Mchunguzi Maalum kwa namba 9220 7555 au tumia baruapepe mail@ombudsman.wa.gov.au

**Naweza kutumia kadi ya ukalimani wapi?**

Kutegemeana na kitu unachotaka kuzungumzia, mashirika ya Serikali lazima yaamue kila wakati kama mkalimani lazima, pengine au labda atumiwe. Wanatakiwa kutumia wakalimani wakati haki yako, afya yako na usalama wako ukiwa hatarini. Mashirika ya Serikali ambayo mara nyingi yanatakiwa kutumia wakalimani ni pamoja na:

- hospitali za serikali
- vituo vya polisi
- mahakama na vituo vya sheria
- shule za Serikali
- ofisi za nyumba za serikali

Unaweza pia kutumia kadi yako kwenye halimashauri yako ya mji.

Unaweza pia kuangalia kama kitongoji chako kina madaktari na mafamasia wowote ambao wameingia mkataba kutumia huduma za ukalimani za bure zinazogharimiwa na Idara ya Uhamiaji na Uraia.

Kama wewe husikii au unasikia kwa shida, wakalimani wa Auslan wanatolewa kwenye mikutano binafsi ya afya na shirika la taifa la Auslan na huduma ya malipo (NABS) bila gharama yoyote kwako. Unaweza kuwasiliana na NABS kupitia tovuti yao ya: www.nabs.org,au

**Siwezi kutumia Kadi yangu ya Ukalimani wapi?**

Mashirika mengi binafsi na biashara mbalimbali hazitaweza kutoa huduma ya mkalimani.

Mashirika kama vile hospitali binafsi na zahanati, shule binafsi, vituo vya sheria binafsi na mashirika ya usafiri binafsi wanaweza kuwa tayari kuandaa mkalimani, lakini wanaweza kukuomba ulipie gharama ili utumie mkalimani.

Kama wewe husikii au unasikia kwa shida, watoaji wa huduma za shule binafsi wanatakiwa kukupatia mkalimani chini ya Sheria ya Ubaguzi ya Walemavu (Viwango vya Elimu).

Tafsiri za brosha hii katika lugha kadhaa, na habari kuhusu Sera ya Huduma za Lugha za Australia ya Magharibi, zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Maslahi ya Tamaduni mbalimbali (OMI):www.omi.wa.gov.au

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na OMI kwa simu namba 6552 7300 au barua pepe

harmony@omi.wa.gov.au

Shukrani: Ofisi ya Mambo ya Utamaduni Mbalimbali inashukuru ruhusa ya Kamishna ya Victoria ya Utamaduni Mbalimbali kuweza kurekebisha kijitabu cha Kadi ya Ukalimani ya Victoria itumike Australia ya Magharibi.